# CTI wazindua utafiti wa biashara, wataka mabadiliko

Na Mwandishi Wetu



SHIRIKISHO la Wenye Viwanda (CTI) limeelezea haja ya kuendelea kutengeneza mazingira bora ya biashara ili kufanya bidhaa zinazozalishwa nchini zikiwemo za huduma kushindana kimataifa.

Kauli hiyo imetolewa juzi usiku na Mkurugenzi Mtendaji wa CTI Christine Kilindu wakati wa uzinduzi wa taarifa ya hali halisi ya mazingira ya kibiashara nchini.

Taarifa hiyo ni matokeo ya utafiti uliofanywa kwa wafanyabiashara na wawekezaji nchini kwa mwaka jana .Taarifa hiyo ni ya nne tangu CTI kwa kushirikiana na BEST-AC katika kutafuta suluhu kwa matatizo ya biashara nchini.

Katika taarifa hiyo mambo manne yalielezwa kukwamisha hali bora ya uwekezaji nchini. Mambo hayo ni tatizo la nishati ya kuaminika, uhafifu wa barabara, rushwa, upatikanaji